Mnamo tarehe 8 Marsi 1993

Wamama kasherehekea siku kuu yao

Kila mwaka wamama washerehekea siku kuu yao mnamo tarehe 8 marsi katika furaha kwa shangwe na vigelegele ulimwenguni kote ingawa magumu yatezamiwa kuwaangamiza. Kuhusu siku hiyo, hapo majuzi muda wa siku tatu akina bibi walionya kwa umma hapa mjini Bukavu mambo kazaa kwa kufikilia maendeleo yao.

Kulingana na siku kuu hiyo, mkutano muhimu kaendeshwa kwenyi chumba cha michezo na maonyesho cha parokia mtakatifu Fransisko Xaveri ya mtaa ya Kadutu. Mkutanoni wa siku ya sita tarehe 6 marsi, wamama waliweza kutatua na kujifikiri mambo mengi kuhusu maendeleo ya mwanamke. Hotuba, nyimbo na mchezo wa "sketch" kafanywa kwa kuonya hali aishi mwanamke kwa siku ya leo. Maandamano kaendeshwa siku ya Mungu tarehe 7 marsi yakihimizwa na *kikundi cha wanamuziki wa askari-jeshi. Pia makusudio na majawabu kazaa kachukuliwa* ili kubadilisha hali ya mwanamke na kuheshimisha utu wake. Sherehe za mwisho ziliendeshwa kunako chumba cha michezo cha chuo "Chirezi" mtaani Ibanda, siku ya kwanza tarehe 8 marsi, siku kamili ya kumbukumbu hilo.

Kwa kweli, siku ya sita tarehe 6 marsi katika mkutano wao, wahuzuriaji waliweza kusikiliza kwa hekima na utaratibu maelezo muhimu kuhusu "hali ya mwanamke na mendeleo" pia mazimio kachukuliwa na tume mbalimbali kunako mkutano mkuu wa kitaifa kuhusu mwanamke. Maelezo yaliyotolewa yalielekea hasa hali ya mwanamke na maendeleo, hali ya mwanamke mkulima, kama vile mama wa nyumba, mwanamke mfanyabiashara, mwanamke mwenyi elimu, mkuu wa jamaa, hali ya binti kwenyi shule kuu, haki na bahati ya mwanamke bila kushau maarifa ya mwanamke katika vita aendesha kwa kugombea haki na utu wake katika nchi mbalimbali.

Baada ya kazi kaendeshwa na makusudio kazaa kachukuliwa na kutolewa. Kati ya majawabu na makusudio kachukuliwa ni kama vile : kuundwa na kuhumiza vikundi na miungano ya wanawake na umoja wao ili kuwahimiza wagombee faida zao, kuhimiza wanawake kujiunga pamoja, kusaidiana na kupendana. Kuundwa kwa vikundi vya mkazo na vya kugombea haki za mwanamke, kuamsha zamiri ya mwanaume na kumuadibisha kulingana mabadiliko yafaa na bora kwa kufikilia hali ya maisha mazuri ya mwanamke katika vikundi vya kidini, masomo,miungano na vikundi vyote vyenyi kupendelea maendeleo ya mwanamke. Kwani, wakati wa mikutano kafanyika ilichunguzwa mambo mwanamke anayo kwali lazim'a na kutafuta majawabu na njia bora kwa kufikilia hali bora. Ni hivi ilikusudiwa kuundwe kamati moja ya kufuatilia utimizo wa mjawabu na makusudio. Matukio yatachunguljwa baada ya mwaka moja ama tarehe 8 marsi mwaka kesho. Itakujiswa pia kuwa akina mama walionya kuwa ni mara haba mke mwenyi elimu na ambaye hatumike na ashinda nyumbani kuzungumza na kutoleana mawazo fulani fulani na bwanae, mwanamke hashurulike na habari zatolewa na utamaduni, huyu atumika muda wa saa 16 pahali za saa 8 kawaida kwa siku, ili mke apate kazi mahali yahitajika yafaa aonyeshe kwanza kibali cha bwanae, wanaume wengi kutokana na ukuu wao wa jamaa, wagandamiza wake wao wakitia msimamo wa kuwa hakuna jambo nzuri mke aweza kufanya. Pia kina baba wengi watwika mapaswa yao mabegani mwa wake wao, baada ya kifo cha mme, mali na watoto yanyanganywa na jamaa lake anayerizi amfukuza mama mjane mikono mitupu. Kitendo ambacho chaenda kinyume cha sheria kuhusu jamaa.

Kumbe kuhusu haki za mwanamke na mapaswa anayo kutokana na siasa ya kidemokrasia yaanza kuota mizizi nchini ni vema wanaume wafanye angalisho na wawe tayari kuwatolea akina mama majawabu kamili kwa malalamiko yafanywa.

André Bisimwa L-B. Tsorou

Tuzungumze

Udemokrasia upi katika makanisa za kikristu

Siku hizi nchini Zaïre watu wote wajiuliza kama katika makanisa ya kikristu, hizo za kiprotestanti na lile la Kimbangu, zinazo tetea na kutaja mara na mara jina la mwokozi wetu Yesu Kristu, udemokratia upi na utaingia siku gani.

Kwa kua udikteta, ubaguzi wa kabila, upokonyaji wa feza, ulozi na uchawi na hata pia uongo ndivyo vyaongoza makanisa mengi jimboni mwa Kivu ya Kusini na hata nchini kote Zaïre. Siyo makanisa yote, ni vema tukamilishe, lakini mengi, ambayo yaubiri pia mambo ya siasa kanisani ao mkutanoni kwa jina la Yesu ! Haibu !

Makanisha yanayojipatisha haya na kujifezehesha sana ni yale ya Kimbagu (EJCK) ambavo yaongozwa kijamii tangu baba mpaka watoto na kuhutubia siasa kanisani siku hizi pale Kinshasa. Na pia, tukumbusheni, kanisa la kiprotestanti (ECZ) ambao uongozi ni wakudumu milele mpaka hapo atafariki mzee Bokeleale "Papa Bok" na wasimamizi wake jimboni na wengineo waheshimiwa (reprÇsentants) waongozao mashirika (communautÇs) na makanisa vijijini. Wote hao waongoza makanisa wanazo pewa mamlaka ya usimamizi kidikteta wakikataa ukombozi ao mabadiliko yoyote mpaka hapo kifo kitapata kuwakumba.

Mambo kama hayo yametangazwa katika kitabu kilichoandikwa na pastori mkuu Philippe Kabongo-Mbaya, mjini Paris nchini Ufransa kunako nyumba ya kuchapa vitabu iitwayo Karthale. Kitabu hicho ni chakusomwa na wakristu wote wa Zaïre ili waondoke katika ukoloni wa wakubwa wa makanisa nchini wanao unga mkono udikteta wa raïsi Mobutu ambaye kawatesa watu nchini mda wa miaka 30 sasa, kwa maneno na mafundisho pia vitendo vibaya alivyo tenda binafsi na mara nyingi akiungwa mkono na wapadri wachafu kama vile wapastori wapenda pesa na cheo ya milele.

Tukichungua vizuri, wasimamizi wengi wamakanisa za kiprotestanti, mapastori wapenda-raha na wasimamizi wa miradi ya maendeleo ni wale waliosoma masomo mafupi. Na wengi hawakusoma. Karibu wote ni wazee sana ao wenyi umri wa miaka hamsini, sitini na zaidi. Watu hujiuliza kama wazee wale ambao wengi waendesha kazi zao kikabila na kirafiki watumika mara na mara wakizunguukwa na wandugu zao, washemeji, watoto, wajomba, watoto wa shangazi ao wa ndugu yeyote wanayetoka naye mkoa ao mtaa moja na wanaye sumulia lugha moja ya kiasili wataka nini.

Ni hapo watu wameona kunako mkutano mkuu uliofanyika mjini Kinshasa wasimamizi wamakanisa hizo hawakutoa maoni, yao, hawakutetea kitu kama wahuzuriaji wengine. Mara na mara walionekana wenyi kulala wakati watu wenyi masomo mengi, maarifa na pumzi ya ujana walikuwa wakipigania hali mpya ya udemokrasia itakayo ruhusu raia kuishi katika uhuru na udemokrasia kulingana na hali ya mabadiliko inayo itajiwa inchini.

Jamhuri ya Tatu, waomba waamini wa makanisa hizo, yapaswa kuongozwa na vijana, mapadri, na askofu, mapastori na wengineo wasimamizi wa makanisa jimboni hata vijijini. Sababu wazee waitwao wa "dinosaures", wale waliopokonya feza kutoka nchi za Ulaya (Suedi, Norvejia, Ugermani...) na Amerika kwa maendeleo ya masomo na makanisa, sherti waondoshwe madarakani na kutupwa gorogoroni. Ni hiyo, kabla ya kurudisha mali walioiba. Ni mali iliyo waruhusu kujenga nyumba nyingi na kubwa kushinda kanisa wanazoziongoza na gari za umaridadi wakizarau waamini walio wafyonza mda wa miaka mingi.

Wale wasimamizi wamakanisa waliotumia pesa za matoleo, sadaka ama "sinsani" na chakumi kwa uchuuzi wa zahabu, safir na almasi wapigwe bakora ya udemokrasia. Kwa sababu yajulikana kama wengi kati yao wamefanya uchuuzi wa kimagendo (fraude) na kuelekeza madini kachimbwa nchini mwetu katika nchi za kigeni.

Kanisa la Kimbagu ambalo lataja jina takatifu la Yesu mjini Bukavu tangu sasa miaka thelatini na zaidi lashindwa kujengwa na vijana waendelea kutoa malalamiko yao ili mabadiliko yafanyike haraka. Sherti mti ao mtu asiyetoa matunda aangushwe na kugombolewa kidemokrasia.

Jambo la kusangaza na kuuzikisha zaidi ni kuona sasa kama ulozi, ukahaba, uongo na ubaguzi wa kikabila wadumu katika makanisa zetu jimboni. Makanisa ambazo siku hizi zaota kama uyoga wa masika. Msihukumu msije mkahukumiwe ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa, yasema maandiko matakatifu (Mathayo 7:1). Lakini Biblia yasema pia (Mathayo 6:33) kama ni vema kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na Kazi yake. Maandiko matakatifu yanayotukataza kuhukumu wengine hairuhusu pia wasimamizi wa makanisa kutenda mabaya, kutumika kikabila na kutupilia mbali vijana na kuwaona kama maadui ama moto wa kuotea mbali.

Basi, waamini wakristu ; fanyeni angalisho. Mda wa miaka mingi samaki kubwa zimemeza samaki ndogo kanisani. Wasimamizi kawatuma watoto na ndugu wao kikabila kunako Univasti Ulaya na katika masomo makuu ya biblia nchi za ugeni na mahali pengine ili waje kuwagomboa hapo kifo kitakapo waondoa madarakani. Wapastori wazee(dinosaures) hawako mbalimbali na wazee wanasiasa waliobomoa nchi na roho zetu wakati wa Jamhuri ya Pili ya udikteta. Fungueni macho msije mkatawaliwe mara ya pili !

Imata Raphaël Déwen

JE, UMESIKIA ...

Kwamba
shirika "SNEL" kapigwa bumbuazi mtaani Bagira ambako vijana kapinga shirika hilo kuchukua chombo moja cha kugawa moto wa stimu mtaani mwao na ambacho katezamiwa kupelekwa jimboni mwa Zaäre ya Juu ? Ya semekana kwamba imekuwa sasa zoezi ya kuchukua "mali ya jimbo la Kivu ya Kusini na kuyabeba majimboni mengine kama vile halina lazima ya mali yake. Mfano moja mwengine muhimu ni kuona chombo kimoja cha radio Bukavu kuchukuliwa na kutumwa jimboni mwa Shaba. Ingawa kweli, jimbo la Kivu ya Kusini halipewe chochote na majimbo mengine. Ebu ! Kumbe ni hatari hapo mekesho tujionye kama wafungwa wasio weza kupata msaada.

Kama
mambo hayaongoke kwenyi kliniki ya Bukavu ? Eti huko mgangakiongozi wa kituo hicho cha matibabu hasikilizane na mmoja kati ya viongozi wa vyumba vya kazi. Hasa kiongozi mwenyi kuhusika na feza. Yajulishwa huko kuwa wote wawili kapewa madaraka bila kutegemea kanuni za uongozi wa kazi toka wizara ya Afia. Ingawa watumishi hawajapokea mishahara yao tangu mwezi wa desemba mwaka jana, mganga kiongozi wa kliniki kamuachisha kazi kwa muda msaidizi wake baada ya kukataa kwa huyu kumuunga mkono katika magendo ya kununua dawa. Eti duka moja la dawa hapa mjini mkoani Nyawera lahimiza magendo hayo likitoa stakabazi zenyi kiasi cha mwende mukaone kwa malipo ya dawa zauzwa. Magendo hayo yamwinisha nakumlisha mganga kiongozi huyo. Hayo ni manunguniko ya bwana Kulumushi ambaye kamshitaki mkuuu wake wa kazi kwa mganga mchunguzi jimboni ili kachungue kwa karibu jambo hilo na kutoa hukumu.

Kwamba
shirika "Regideso" lashutushwa na ofisi yake mtaani Kadutu ? Je ? Kwa kuwa tu vibambazi vyaonya vistari vya kubomoka ingawa ofisi hiyo kajengwa bado siku si nyingi. Imeonekana kweli kuwa kanuni za ujenzi hazikuheshimiwa. Na hiyo kutokana na masililizano kafanywe kati ya viongozi wamoja wa shirika "Regideso" jimboni na mtaalam moja wa ujenzi wa hapa mjini Bukavu. Ubovu waonywa kwenyi ukuta haukamilishe ujuzi wa mtaalam huyo. Twazani kama viongozi wa shirika hilo watachungua kwa makini tatizo hilo. Bali pia watumiaji wa maji yatolewa na shirika "Regideso" walipinga na kukataa kulipa stakabazi katumiwa. Kwani malipo yaombwa hayalingane na mishahara wala pato lao.

Kuwa
wakuu wa serkali jimboni hawakuelewana na kamati ya ungozi wa sherehe kaendeshwa wakati wa kumbukumbu la siku kuu la mwanamke njini Bukavu ? Hapa mjini, akina mama wanongonezana kuwa hakuna hata mkuu moja wala mke wake kahuzuria sherehe hizo ingawa makuu na wake wao kaalikwa. Wakuu wamoja kataka hata kuwashawishi wenzio eti kundi la askari wapiga muziki wasihimize maandamani katayarishwa na hata pia wakawakatalia kuendesha sherehe zao katika Jumba la "CEPGL". Hasa pia hawakufurahishwa kusikia jina la padri moya kati ya kikundi cha wahotubiaji. Hum ! Labda kuna kitu chawazungusha ubongo.

Eti
mtaani Ibanda kunako barabara yenyi kujielekeza Uvira, tangu mwaka moja sasa waamini wa kanisa moja na kinachosangaza ni wa kabila moja "Watutsi", wasemvyo huko, wakutana kila siku ya Mungu ? Aah ! Eti ndugu hao katika kristu watoka mitaani kote mjini Bukavu na hata mjini Cyangugu (Rwanda). Loo ! Eti pia hiyo ndiyo namna bora ya kuonya kwa umma njia yaonekana ndefu kwa hao hawajui kuungana kindugu na kujibagua kikabila. Eti tubaki wakristu, tuugane lakini tukiwa mbalimbali na wengine.

Kuwa
maandamano mengi yafanyika mjini Bukavu na hata vikartasi vingi kubandikwa, kutupwa huku na kule na waanfunzi ao walimu wao kazaa kwa kupinga viongozi wa shule zao kwa kufikilia nia na faida zao ? Watu wengi wazania ukomo wa maandamano na vitendo vyaendeshwa ni kupata nyumba, vyeo ao mawazo wanayo kuhusu misaada ya feza yatolewa mwaka huu na wazazi. Ingawa maelimisho yao hayaaminiwe kweli. Je, hakuna tena ginsi wala njia nyingine ya kutoa malamiko kunako shule zetu ambako wote wajidai kuwa wapenda mabadiliko yafanyike nchini ? Kwa kweli iliyo haki ni kuona maadibisho yafanyike kwa udemokrasia yafanywe ummani na haraka kwa kufikilia kipindi cha mpito bora.

Kwamba
mganga moja kakazwa kutoka katika nyumba ya serkali apanga mtaani "Ibanda bila huruma na hao wanaohusika ? Yasemekana kuwa viongozi wa serkali jimboni wataka kugeuza nyumba hiyo mahali pa kuwapangisha na kuwapokea wageni wa heshima. Ndiyo, lakini hakuna hata kitu kimoja chatezamiwa kushurulikiwa ili mganga huyo na jamaa lake wapate makao. Tume lenyi kuhusika na kugawa nyumba za serkali lamshawishi akae nyumba moja na mtumishi moja wa serkali ambaye kaachishwa huko. Lakini imeonekana kama ni vigumu jamaa mbili hizo kuishi pamoja ingawa wanamemba wote ni wakaaji wa mji moja.

Kuwa
chumba cha sinema hapo zamani "Ciné Palace" na baadae "Ciné Rwacico" katengenezwa upya na kupewa jina la Maison du Parti(Chumba la Chama)"? Kwa sasa wapitanjia hujiuliza baada ya Chama-Serkali kuvunjwa, jina gani chumba hilo litapewa kwani wamekwisha kuvuta jina katwika. Basi kwa kuwa jumba hilo katengenezwa upya kwa kuwapokea maraïs na nchi memba wa Jumuhuria la kiuchumi la nchi zinazopakana na mazima makuu "CEPGL", jimbo hilo liitwe maramoja "Maison de la CEPGL".